


USIMULIZI WA HADITHI

Chombo cha Kuendeleza amani na Usomi



Education makes a world of difference

Haki ya Kunukuu @ 2011 – Feed the Minds

Feed the Minds

Park Place, 12 Lawn Lane, London SW8 1UD, United Kingdom

info@feedtheminds.org

www.feedtheminds.org

Kimeandikwa na: Katy Newell-Jones na Rosie Crowther

Mhariri wa Nakala: Pelagie T. Gichanga

Michoro-elezi na: Anne Wilson

Mtindo wa Jalada: Alphonse Mutisya

Chapa na: Alpace Graphics Designers

Kijitabu hiki kimeandikwa na Katy Newell-Jones na Rosie Crowther wa Feed the Minds wakitungia hadithi walizokusanya kutoka kwa washirika wetu:

Advocacy for Social Development and Environment - Uganda (ASDE-U)

Femmes et Education des Adultes (FEDA)

Peacebuilding, Healing and Reconciliation Programme (PHARP)

Sudan Evangelical Mission (SEM)

Tatua Communication

Youth with Physical DisabilityDevelopment Forum (YPDDF)

Michoro-elezi na Anne Wilson

Mwakaribishwa kutengeneza nakala za kijitabu hiki na kukitungia katika warsha. Hata hivyo, tafadhali, tambulisha Feed the Minds kila wakati unapokitumia. Pia tunakaribisha maoni kuhusu ya kijitabu hiki na jinsi kilivyotumikiwa. Tafadhali tuma maoni yako kwa info@feedtheminds.org

Nakala zingine za kijitabu hiki zinapatikana kutoka kwa SEM pia PHARP, na pia kwa kusafura tuvuti ya Feed the Minds www.feedtheminds.org

Feed the Minds

Park Place, 12 Lawn Lane, London SW8 1UD, United Kingdom

Email: info@feedtheminds.org

www.feedtheminds.org

Peacebuilding, Healing and Reconciliation Programme (PHARP)

Matasia/ Kiserian Road, Oloosurutin, Supreme Business Centre

P.O Box 15324, GPO 00100, Nairobi, Kenya

Email: info@pharp.org

www.pharp.org

Sudan Evangelical Mission (SEM)

P.O Box 367 Juba, South Sudan

P.O Box 8423, 00100 GPO, Nairobi, Kenya

Email: sem@maf.or.ke

[sem1998.mundri @ gmail.com](mailto:sem1998.mundri@gmail.com)

Advocacy for Social Development and Environment - Uganda (ASDE-U)

P.O Box 634, Arua, Uganda

Email: asdeuhassan@yahoo.com

Femmes et Education de Adultes (FEDA)

Kazimia, Fizi District, South Kivu, Democratic Republic of Congo

P.O Box 1268, Kigoma, Tanzania

Email: feda.secretariat@yahoo.com

Yaliyomo

Shukrani	5
Vifupisho	6
Utangulizi	7
Kwa Nini Mwongozo huu Ukaandikwa?.....	8
Mwongozo Huu Waweza Kutumiwa Vipi?	8
Kuunganisha Usimulizi wa Hadithi, Kusoma na Kuandika	8
Maneno Muhimu	9
Washiriki wa Kikundi cha Usimulizi wa Hadithi Watanufaika Vipi?	9
Ni nini Kinachoweza kufanya Hadithi Iwe ya Kuvutia?	10
Jinsi Gani Tunaweza Kuwezesha Usimulizi wa Hadithi?	11
Usaidizi wa Maandishi	19
Hadithi na Mashairi	21
Vita ni Vikatili: Yotoma James	22
Kupambana na Unyanyapaa: Gasi Stella	23
Anyimwa Elimu kwa ajili ya Ndevu Zake: Christopher Malone	24
Je, Nilichagua Vyema? Gertarude Philip	25
Teksi, Tafadhali! Henry Nyombi	26
Nalia Kinyamavu: Judy Amunga	27
Majirani Katika Amani: Boniface Ambani	28
Elimu ni Ufunguo wa Amani: Felicien Nemeyimana	29
Wanawake Wamesimama Pamoja: Katy Newell-Jones	31
Uponyaji Kupitia kwa Msamaha: Ekombe Athuman	32
Sehemu Tano za Mpango wa Feed the Minds	33
Tajo	34

Shukrani

Kijitabu hiki kilitolewa kusaidia mradi uitwao "**Kuponya Sononeko kwa Kutumia Usimulizi wa Hadithi, Kusoma na Kuandika**" unaofadhiliwa na Feed the Minds (FTM) kwa ushirikiano na Peacebuilding, Healing and Reconciliation Programme (PHARP) na Sudan Evangelical Mission (SEM).

Shukrani mahsusи ziwaendee washiriki wa warsha za Sudan Kusini na Kenya za mwaka 2010 kulikoshirikishwa wingi wa hadithi hizi, na hususan waliochanga hadithi zao:

Adam Sach (FTM)	Jane Akinyi (PHARP)
Ambu Daudi George (SEM)	Judy Amunga (Tatua Mawasiliano)
Boniface Ambani (Utukufu School)	Julius Dobo (SEM)
Célestin Buyore N-Bose (PHARP)	Katy Newell-Jones (FTM)
Christopher Malone (SEM)	Lillian Aya Samweli (Idara ya Elimu Mundri Magharibi, Sudan Kusini)
Cornelia Kunze (PHARP)	Linet Anindo (PHARP)
Daniel Okello (Harvest Impact Ministry)	Michael Augustus (SEM)
Ekombe Athumani (FEDA)	Pelagie Tuyisenge (PHARP)
Felicien Nemeyimana, (PHARP)	Peter Onyango (PHARP)
Gasi Stella (ASDE-U)	Rosie Crowther (FTM)
Gerald G. Gichanga (PHARP, CITAM)	Ruth Kanamugire (PHARP)
Gertarude Philip (SEM)	Ruth Patta (PHARP)
Grace Bunga (PHARP)	Susan Mukarurema (PHARP)
Gulliver Ishmaeli (SEM)	Yotoma A. James (SEM)
Henry Nyombi (YPDDF)	

Tunashukuru wafadhili wa Feed the Minds ambaо waliamini mradi huu na ambaо bila ya wao warsha tulizozitaja hazingelifanyika, wala mwongozo huu kuandikwa.

Vifupisho

ASDE-U Advocacy for Social Development and Environment - Uganda

CITAM Christ Is the Answer Ministries, Kenya

FEDA Femmes et education des Adultes (Wanawake na Kisomo cha Watu Wazima), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo

HIV& AIDS Ukimwi (Virusi Vinavyosababisha Upungufu wa Kinga katika Mwili wa Binadamu)

YPDDF Youth with Physical Disability Development Forum, Uganda

Utangulizi

Usimulizi wa hadithi una nafasi muhimu katika jamii ya Afrika, hasa katika familia. Kitamaduni, watoto kujifunza kuhusu mila, dini na utamaduni wanaposikiliza hadithi kutoka kwa wazazi wao. Hadithi huwasaidia watu kuelewa dunia na watu wengine. Hata hivyo, baadhi ya hadithi kuhamasisha ukabila, na hadithi zinaweza kutumika kutekeleza dhuluma na mashinikizo. Hivyo basi, uteuzi makini ni muhimu.

Hadithi miongoni mwa watu wazima mara nyingi hutumika kwa kuburudisha, bali pia zinaweza kuwa chombo cha nguvu cha kujenga amani katika familia na jamii zilizogawanyika. Hadithi hutoa fursa ya kutatua migogoro na kusaidia watu kusamehe na kupatanishwa.

Usimulizi wa hadithi unaweza kuwa wa thamani katika kuwafariji wanao omboleza msiba au hasara zozote. Msimulizi wa hadithi anaweza kunufaika kwa kuhisi kuwa hayuko 'peke yake' na ya kwamba kuna watu 'waliosikiliza' masaibu yake. Anayesimuliwa anaweza kusikia na kuelewa matukio kupitia kwa macho na masikio ya mtu mwengine. Hatua za usumulizi wa hadithi zikiwezeshwa kiustadi, zinaweza kusaidia jamii kuandaa mipango ya uponyaji na maendeleo.

Sanaa ya usimulizi wa hadithi imekuwa ikipotea katika baadhi ya jamii kwa njia ya vita na migogoro, kutokana na kuvunjika kwa familia au kuongeza kwa teknolojia. Ili kurejelea dhamani iliopotezwa na sanaa ya usimulizi wa hadithi katika jamii, warsha zilifanywa katika

Sudan Kusini na Kenya, chini ya uongozi wa Feed the Minds kwa kushirikiana na Sudan Evangelical Mission (SEM) na Peacebuilding, Healing and Reconciliation (PHARP).

Washiriki waliletwa kutoka Sudan Kusini, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Uganda, ambao wote kuwa waliadhirika na vita na migogoro ya hivi karibuni. Warsha alisistiza nguvu ya usimulizi wa hadithi katika kujenga amani, kuponya sononeko, elimu ya uraia, utatuvi wa migogoro, kuimarisha elimu, na nafasi yake katika jamii. Mojawapo wa mandhari ya manufaa ya warsha hizo ilikuwa majadiliano kuhusu jinsi ya Kuandaa Usimulizi wa Hadithi, ambao ndio msingi wa kijitabu hiki.

Mwishoni mwa warsha, hadithi zilikusanya na mwongozo ukatengenezwa utumiwe na wasimamizi katika makanisa na jamii ukilenga waathiriwa wa sononeko na ubaguzi na wale waliotengwa kwa sababu ya migogoro.

Mbona Mwongozo Huu Ukaandikwa?

Feed the Minds, PHARP na SEM wamejitolea kutumia usimulizi wa hadithi, hususan kama chombo cha kujenga amani. Kujenga amani hujumuisha uponyaji wa sononeko, utatuzi wamigogoro, maridhiano, kuimarisha jamii na elimu ya uraia. Kujenga amani kunahitajika katika jamii zote wala sio zile zinazotoka kwa vita au migogoro. Palipo na ubaguzi na unyanyapaji dhidi ya watu wanaoishi na UKIMWI, watu wenye ulemavu, au vikundi vingine viliyotengwa, kujenga amani kaweza kujenga imani, kuwawezesha watu binafsi na kuimarisha jamii.

Hadithi zaweza kuwa njia ya kuwawezesha watu waliofanyiwa ubaguzi an kupata kiwewe, unyanyapaji au migogoro kusimulia hadithi zao na kusikilizwa. Wanaweza kuleta ufahamu kuhusu masuala nyeti kama ubakaji, kufurushwa kutoka kwa makazi yao, hali ya wasiwasi baina ya makabila au ukosefu wa uwakilishi wa wanawake. Wanaweza kuwa wa muhimu hasa katika madarasa ya kisomo na duru katika kuhamasisha washiriki kubadilishana matukio katika maisha yao, kujifunza kusoma na kuandika kuhusu masuala yaliyo muhimu kwao na kupata ujasiri wa kuchukua hatua katika maisha yao.

Wawezeshaji wengi wa vikundi wanajua thamani ya hadithi na usimulizi wa hadithi lakini wanakosa ujasiri na umahiri wa kuzitumia. Tunaamini kuwa kila mtu anaweza kutumia usimulizi wa hadithi. Mwongozo huu kimeandikwa kutoa ushauri, vidokezo na mifano.

Mwongozo Huu Waweza Kutumika Jinsi Gani?

Tunawahimiza wawezeshaji kuchukuliamwongozo kuwa wa vidokezo na mapendekezo. Hadithi katika kijitabu hiki zinaweza kutumiwa jinsi zilivyoandikwa hapa. Hata hivyo, katika uzoefu wetu, watu katika vikundi wanaweza kunufaika zaidi wanaposimulia hadithi zao wenyeye, wanapozijadili baadaye na kujifunza kutokana na masaibu ya kila mmoja.

Kuunganisha Usimulizi wa Hadithi, Kusoma na Kuandika

Mara kwa mara hadithi husimuliwa kwa maneno bila ya kuandikwa. Hata hivyo, tunaona kusoma na kuandika kuwa mambo muhimu katika uwezeshaji. Tunawahimiza wawezeshaji wanaotumia usimulizi wa hadithi ya kukusudia kuzichanganya na kusoma na kuandika kidogo. Kwa wale ambao husoma na kuandika kwa urahisi, kuandika hadithi yetu kunaweza kusaidia kufafanua tunachotaka kusema. Pia, kuwasikia watu wengine wakisoma hadithi zetu kunaweza kutusaidia kuona uzoefu wetu kwa mtazamo tofauti.

Kwa wale wanaopata kusoma na kuandika kuwa kugumu, kuandika hadithi zao, mara nyingi kwa usaidizi kutoka kwa wengine, kunaweza kuwa njia ya kujifunza maneno mapya na kufanya mazoezi ya kuandika, lakini muhimu zaidi, inaweza kuwa ni njia ya kuthibiti mawazo na uzoefu wao. Wao pia wanaweza kuona mawazo wenyewe juu ya karatasi, ijapo kuwa kwa urahisi, na kuhisi kujivunia kuzungumzia mawazo yao kwa njia ya maandishi.

Muhimu Maneno

Washiriki wa warsha nchini Sudan Kusini walichaguwa maneno yafwatayo 12 yaliyotokea katika hadithi vingi. Kila hadithi katika kijitabu hiki inahusiana na angalau maneno mawili muhimu. Vikundi vingine vyaweza kusoma hadithi hizo na kuchagua maneno mengine muhimu yaliyo na maana kwao.

- | | |
|------------------|---|
| ◆ Elimu ya uraia | ◆ Simanzi |
| ◆ Migogoro | ◆ Uponyaji |
| ◆ Ubaguzi | ◆ Hasara |
| ◆ Makazi yao | ◆ Msamaha |
| ◆ Amani | ◆ Unyanyapaji |
| ◆ Maridhiano | ◆ Ukosefu wa usawa wa kijinsia/
wanawake |

Washiriki wa Kikundi cha Usimulizi wa Hadithi Watanufaika Vipi?

Inaposimuliwa katika makundi yanayounga mkono, 'msimulizi wa hadithi' anaweza kunufaika kutokana na mtu mwingine anayesikiliza na kushuhudia matukio katika maisha yake, na kuwashirikisha katika yanayomsonga na mateso yake. Usimulizi wa hadithi unaweza kumwezesha mtu kusema ukweli wake kwa mara ya kwanza na kutambua maumivu aliyokuwa akiishi nayo. Walioendeleza ghasia pia waweza kunufaika kutokana na usimulizi wa hadithi kwa kusema matendo yao, jinsi wanavyohisi kuhusu matendo hayo na zaidi shinikizo wanazohisi zinawasonga wakati huo.

'Msikilizaji' anaweza anaweza kunufaika kwa kusikiliza matukio katika maisha ya mtu mwingine yaliyo sawa na yao wenyewe ambayo inaweza kupunguza hisia za kutengwa au hatia na kuanza kujenga daraja. Wanaweza kuanza kuona kwamba wengine pia wanakabiliwa na changamoto kama zao kila siku; labda ni picha za aliyotenda kuwa mawazoni, labda jinamizi, labda ni kutokuwa na uwezo wa kutembelea mahali fulani, kama bomba la maji palipotokea tukio paya, labda ni matatizo katika kumpenda mtoto aliyebakwa.

'Msikilizaji' anaweza pia kunufaika kwa kusikiliza hadithi za matukio katika maisha ya watu wengine ambazo ni tofauti sana na yake wenyewe. Hii yaweza kusaidia watu kuwa na mtazamo tofauti katika migogoro, wakati mwingine kuwasaidia watu kutambua matokeo ya matukio katika maisha yao wenyewe. Kwa mfano mwanamke ambaye alibaki katika kijiji chake wakati wa migogoro, kwa kujificha, ameogopa, akishudia ukatili, hali akisaidia manusura, kuwachukulia majukumu wengine hali hana yejote katika familia aliyebaki, kukabiliana na hasara yake mwenyewe, akizungumza na mwanamke aliyekimbia, akaishi miaka katika kambi ya wakimbizi, akiwa mara nyingi na njaa ya chakula na heshima, na kutegemea misaada isiyobainika kutoka kwa wahisani na mashirika yasiyo ya serikali, hali akihofia ubakaji na vurugu. Wanaweza kusikia hadithi za kila mmoja na kuelewa mateso mengine wamepitia. Muhimu pia ni kwa wanawake hawa kusikia hadithi ya wale ambao

huenda ikawa walitekwa nyara, au wakaamua kuwa wapiganaji, na sononeko wanachoishi nacho kila siku ya maisha yao.

Mojawapo wa funguo za matumizi ya usimulizi wa hadithi kwa ajili ya kujenga amani ni njia ambayo msimamizi au kiongozi wa kikundi inasaidia katika tararatibu.

Ni nini Kinachoweza kufanya Hadithi Iwe ya Kuvutia?

Baadhi ya hadithi ni ni za kukumbukwa na huvutia watu waende wakizifikiria kwa siku nyingi, na wakati mwingine hata baada ya miaka mingi baadaye. Hivyo basi, tulijiuliza:

"Ni nini kinaweza kufanya hadithi iwe ya kuvutia?"

Hadithi zinazovutia huelekea kuwa

- Zinaelezea matukio muhimu katika maisha ya msikilizaji
- Hutumia lugha inayoeleweka kwa urahisi.
- Zinashawishi na nizakuaminika
- Zina hisia kiasi
- Haziwaambi wasikilizaji ni yapi ya kufikiria ila huwahimiza kufikiri wenyewe.

Usimulizi wa hadithi unapotumiwa katika vikundi, hadithi zinazopata ufanisi zaidi ni zile zilizo na moja au yote ya yafwatayo:

- Jina linalo vutia
- Ni fupi na dhahiri
- Ni kweli na sahihi
- Kuwakumbusha watu yaliyofanyika
- Ni bayana kuhusualiyeandika hadithi, lini na wapi.

Hata hivyo, tulihisi kuwa njia ambayo hadithi hutumiwa ni muhimu kama hadithi yenye. Hivyo tunakushauri pia usome sehemu inayofuata kuhusu jinsi ya kuwezesha usimulizi wa hadithi.

Jinsi Gani Tunaweza Kuwezesha Usimulizi wa Hadithi?

Hadithi za kuvutia zinaweza kuhadithiwa watu wazima, vijana, watoto, watu wasiojua kusoma na kuandika, viongozi; kwa uhakika, wau wote.

Katika kijitabu hiki tunatumia usimulizi wa hadithi kama kitendo cha kikundi cha kujenga mani, kuponya kiwewe na maridhiano, usimulizi wa hadithi ukitendeka baina ya washiriki wa kikundi. Hatua za usimulizi wa hadithi zina sehemu tatu:

Maandalizi

Pindi

Baadaye

Maandalizi

Ni muhimu kubuni mazingira mema ya kusimulia hadithi. Imani yapasa kujengwa. Mara nyingi watu huhitaji usaizidi ili wajione kuwa wasimulizi wa hadithi. Ambapo usimulizi wa hadithi utatumikiwa kwa kujenga amani ni muhimu kujua kitu kuhusu

- Aina ya migogoro na vurugu iliyo ya kawaida katika maisha ya washiriki
- Changamoto zinazowakabili washiriki katika maisha yao

Mida madhubuti, ramani jamii na michoro ya kibuibui ni vitendo vitatu rahisi vinavyohitaji rasilimali chache ili kusaidia makundi kukiandaa kwa ajili ya kusimulizi wa hadithi. Kila kitendo kinaweza kutumika kwa aina mbalimbali ya vikundi, yakiwemo madarasa ya kisomo ambamo washiriki kujifunzia maneno mapya na kuendeleza umahiri mpya katika kusoma na kuandika.

Katika mida madhubuti uliowekwa, watu binafsi hualikwa kuchora chini au kwa karatasi matukio muhimu katika maisha yao chini ya ardhi au karatasi, kwa kawaida wakitumia michoro wala sio maneno. Baadaye hualikwa kuzungumzia wengine michoro yao na maana yake kwao.

Mida madhubuti yaweza kuwa njia salama na bunifu ya watu kuanza kuzungumza kuhusu nyakati ngumu katika maisha yao kwa kuwa wanaweza kuchagua watakachojumuisha katika mazungumzo na jinsi ya kukizungumzia. Hizi ni njia bora za kujifunza zaidi kuhusu maisha ya watu na changamoto wanazozikabili. Watu wanaweza kuchagua matukio kutoka kwa mida madhubuti yao na kuitumikia kwa kusimulia hadithi kwa maongezi ama maandishi.

Mida Madhubuti

Madhumuni:

Kusaidia washiriki kushiriki matukio makubwa katika maisha yao na kuelewa matatizo na changamoto zinazowakabili wtu wengine.

Kitendo:

- Wakifanya kazi peke yao, washiriki kuchora mida madhubuti inayoonyesha matukio muhimu katika maisha yao, kama vile ndoa au kufurushwa kutoka kwa makazi yao
- Washiriki kutumia muda mtulivu kufikiria kuhusu changamoto kama vite ukame, hasara na vita
- Washiriki watafanya mazoezi ya kusimulia hadithi zao wenyewe katika vikundi vidogo vya watu watatu hadi wanenye wengine wanaposikiliza
- Kikundi kinachagua hadithi moja kuwaambia washiriki wengine
 - Mtu mmoja anasimulia utangulizi wa hadithi
 - Mtu wa pili anasimulia hadithi yenyewe anaelezea hadithi
 - Mtu wa tatu anaelezea kwa nini hadithi hiyo alichaguliwa na nini kinachoifanya hadithi yenyewe kuwa yakuvutia
- Majadiliano ya kikundi kizima kuhusu hadithi ikiwa ni pamoja na haki zilizonyimwa ama kupatikana
- Kundi humulika masomo wanayoweza kujifunza kutoka kwa hadithi na jinsi wanaweza kuwasaidia watu katika jamii zao wenyewe.

Maelezo kwa Mwezeshaji: Kitendo hiki husaidia washiriki kujadili anabainisha shughuli Hii husaidia washiriki kujadili mitazamo tofauti-tofauti na kuelewa maoni ya watu wengine.

Ni muhimu washiriki wasiwe katika shinikizo zozote za kuzungumzia nyakati fulani katika maisha yao, ila wanaweza kuchagua kusema mengi au machache wanavyotaka wenyewe.



Mda Madhubuti katika kijiji kilichovamia na waasi,
Kambia, Sierra Leone, mwaka wa 2001

Na kwa **Ramani ya Jamii**, washiriki hualikwa katika vikundi vidogo, kuchora ramani ya jamii yao wenyewe, halafu kujadili masuala ya msingi, kwa mfano ambapo misukosuko au mgogoro au ambapo wanawake wamo hatarini zaidi.

Kwa kawaida, maandishi hayatumikiwi. Ni michoro pepe yake, ambayo inaruhusu sauti ya watu wasiojua kusoma kusikika vyema na wale wanaojua kusoma na kuandika vizuri. Kitendo hiki kinasaidia watu kuelewa vyema jamii za watu na kuwaona kupidia kwa macho yao. Baadaye, masuala yanatambuliwa. Washiriki huwa maakini sana kusimulia hadithi kutoka kwa matukio ya migogoro katika jamii zao.

Ramani ya Jamii

(Ilichukuliwa kutoka Doe, McCaffery & Newell-Jones, 2004, ukurasa wa 79)

Kusudi:


Kwa washiriki kushirikishiana maarifa ya jamii zao na aina ya migogoro katika maisha yao ya kila siku.

Kitendo:

- Washiriki kuunda vikundi vya watu watatu hadi sita
- Kila kikundi kuchora ramani ya kijiji au jamii yao. Hii inaweza kufanywa chini kwa kutumia vifaa kama vile vijiti na mawe, au kwa kuchora kwa karatasi kubwa.
- Kila kikundi kuweka alama kwenye sehemu muhimu za migogoro katika jamii yao. Watajadili 'visa bayana' na vyanzo vya migogoro.
- Kila kikundi kuzungumza na washiriki wa vikundi vingine kwa njia ya ramani yao.
- Kundi kuchagua aina moja au zaidi ya migogoro ya kujadili na kutafuta suluhisho.

Maelezo kwa Mwezeshaji:

- Kutumia vitu au michoro wala sio maneno, huruhusu kila mtu katika kikundi kuzingatia jamii yao na hauzuii mtu ye yote asiyekuwa msomi.
- Ni muhimu kwa kila mtu kuhisi kuwa ana uwezo wa kuijiunga. Hakuna 'jibu mbovu.' Kuwa huru kueleza mawazo na maoni ni muhimu sana na mawazo ya kila mmoja yanaweza kukubaliwa.
- Kitendo hiki chaweza kutumika kama muundo msingi wa usimulizi wa hadithi katika kikundi, ikifuatiliwa na kushughulikia baadhi ya masuala ya kutambuliwa, na kutafuta jinsi ya kujenga amani.
- Kuchora ramani pia kunaweza kuelekeza kwenye vitendo vingine vya kisomo (Kwa mfano mwanagenzi akizidisha maneno kwa kuandika katika ramani, hupanda kiwango cha kati cha kuandika kuhusu migogoro katika jamii zao).



Ramani ya jamii katika makazi duni ya Kibera, Nairobi, Kenya, mwaka 2010, inayoonyesha hali ya uhasama kati ya jamii za Kikristo na Kiislamu na magenye yakivuka reli, ushindani wa shule na kuzuka kwa mapigano vichakani.

Michoro ya Kibuibui zaweza kutumika kwa kushirikisha matukio na hadithi katika kikundi zaweza kuelekeza jamii kujenga amani na kujiimarisha.

Mchoro wa Kibuibui

Kusudi:

kushirikisha matukio na hadithi kuhusu mandhari maalum.


Kitendo:

- Neno muhimu kuchaguliwa na kikundi na kuwekwa katikati ya ukarasa (Kwa mfano, uongozi, kifo, kupiga kura)
- Washiriki kutaja maneno wanayounganisha na neno muhimu (Kwa mfano, watu, ufisadi, uwajibikaji, wema, kupiga kura, demokrasia)
- Washiriki wanaulizwa kuzungumza kuhusu sababu za kuchagua maneno haya
- Washiriki wanaalikwa kushiriki hadithi ya matukio yao yaliyosababishwa kutokana na neno muhimu na majadiliano.

Maelezo kwa Mwezeshaji:

Wakati wito nje ya maneno, au kutafakari, ni muhimu kwamba maneno ya kila mtu yanahusishwa. Hakuna jibu 'sahihi' wala 'kosa' kwa kuwa watu tofauti tofauti wataunganisha neno muhimu na matukio tofauti tofauti katika maisha yao.

Kitendo hiki kina manufa katika duara ya usomi kwa kuwa kiasli kinaongoza katika kuchagua maneno mapya, kujifunza jinsi ya kuyaandika na kuyaweka katika vifungu vyaa maneno viliyoundwa na washiriki.



Mchoro wa Kibuibui unaoeleza sifa za kiongozi mzuri, kutoka katika warsha ya Sudan Kusini, mwakani 2010

Wakati hadithi zimechaguliwa na kikundi kiko tayari kuzisimulia na kuzisikiliza Mwezeshaji kwa kawaida

- Atachagua mahali pazuri pasipo na matatizo
- Waruhusu washiriki kuchagua watakachosema ili wasihisi kuwa wanashurutishwa kuzungumzia vitu wanavyotarajia kubana
- Hakikisha kwamba msimulizi wa hadithi anajua sababu yako kutaka kusikia hadithi yake na yakwamba anaweza kenena machache au mengi jinsi atakavyotaka
- Hakikisha kwamba msimulizi wa hadithi anajua hadithi yake itawekwa kuwa siri na hakuna mtu mwingine atakayeirudia isipokuwa wanataka ifanyike hivyo.

Pindi

Pindi hadithi inapohadithiwa, imempasa mwezeshaji kuelekeza mawazo kwa msimulizi wa hadithi na pia kundi. Kikundi cha Sudan Kusini kilishauri ifuatayo:

- Onyesha maanani, nia na kusikiliza kwa makini
- Kuwa na huruma na wema moyoni wako
- Muangalie msimulizi wa hadithi macho kwa macho ikiwa yeye anakuangalia
- Epusha utatizi kusiofaa kutoka kwako au kwa kikundi
- Uliza maswali mepesi kwa kutaka ubayana au kutia moyo, ikiwa inahitajika hivyo
- Mruhusu msimulizi wa hadithi kusema mengi au machache jinsi atakavyotaka
- Hisia zikipanda, neno jepesi au papaso jepesi kwa mkono itasaidia
- Kuwa na ujasiri wa kusikiliza; wala usijaribu kufikiria mambo ya kusaidia 'uyaseme'
- Ruhusu muda wa kimya pindi msimulizi wahadithi anapomaliza

Baadaye

Jinsi kikundi kinavyoitikia baada ya mtu amesimulia hadithi inaweza kuwa na athari kubwa sana kwa msimulizi huyo na kwa hatua za uponyaji. Ikiwa usimulizi wa hadithi utatumwa kwa ajili ya kujenga amani na kiwewe mambo yafuatayo ni muhimu:

Fanya

- Mshukuru msimulizi wa hadithi kwa hadithi yake
- Tambua ujasiri unaohitajika kwa kusimulia hadithi zao
- Mruhusu msimulizi wa hadithi kukaa kimya ikiwa anataka hivyo
- Mtie moyo msimulizi wa hadithi kuzungumzia sehemu za hadithi wanazotaka, kabla ya kujadili maeneo mengine
- Peana muda wa kutosha wa kujadiliana baada ya hapo
- Malizia kwa kumpa kila mtu nafasi ya kusema kile walichonufaika nacho kutokana na hadithi.

Kushuhudia hadithi ya mtu kwa kusikiliza na kuunganika na msimulizi wa hadithi ni moja wapo wa manufaa makubwa msikilizaji mzuri anaweza kufanya.

Usifanye

- Usianze kwa kuuliza maswali mengi mara moja
- Usijaribu kupeana ushauri au kupata suluhisho
- Usiwatie moyo wengine kwenda moja kwa moja katika hadithi zao
- Usiende kwa mambo mengine haraka.

Kama msikilizaji wa kazi yako ni si kwa ajili ya kutoa ushauri, kutatua matatizo au kupata majibu.

Wakati wa kutumia usimulizi wa hadithi katika kikundi, himiza kikundi kubainisha masuala muhimu. Msimulizi wa hadithi imekuwa jasiri wa kutosha kuwasimulia hadithi yake: imetupasa kuwa na ujasiri wa kutosha kushuhudia kwa kutambua ikiwa ubaguzi, migogoro au kubakwa kumeathiri maisha ya mtu. Hii ni bora kufanyika katika baina ya watu wawili wawili au makundi ndogo sana ili kuwezesha kila mtu kuwa na nafasi ya kuzungumza kuhusu hadithi wakati msimulizi wa hadithi kivyake anapata muda wa kuketi kimya, au anzungumza kwa mweseshaji.

Saidia kikundi katika kuianisha masuala yanayohusiana na maisha yao. Kwa mfano, kama hadithi inaeleza ubaguzi unaweza kuwauliza kufikiri kuhusu njia ambazo watu mbali mbali wanabaguliwa katika jamii zao. Unaweza pia kuwauliza ikiwa kuna ubaguzi katika jamaa zao, au mahali anapoweza kupata msaada katika jamii hiyo.

Mwisho, ni muhimu kwa upole kumtia moyo kila mmoja kuchukua ujumbe kwao wenyewe kutokana na hadithi iliyosimuliwa, wakijibu maswali.

'Nini nimenufaika vipi?' na 'Nitafanya nini sasa?

Kusaidia Kisomo

Mojawapo wa faida ya usimulizi wa hadithi ni kwamba kila mtu, awe anaweza au hawesi kusoma na kuandika, unaweza kusimulia hadithi muafaka. Feed the Minds imejitolea kusaidia kisomo katika ushirikiano wetu wote na inaendeleza ya Mpango wa Hatua Tano za Kisomo (Tazama Mwisho wa Mwongozo huu) ulio kama kumbukumbu kila tunapo fanya kazi katika jamii ilio na watu walio na umahiri mdogo wa kisomo. Mpango wa Hatua Tano za Kisomo sio kwa ajili ya ratiba ambako duru za kisomo au madarasa yanafanyika, ila ninkwa ushirikiano wa ratiba zote. Katika ratiba zote za kijamii patakuwa na watu walio na viwango mbali mbali via kisomo. Baadhi yao wanaweza kusoma na kuandika kwa urahisi, hali wengine wanaweza kuwa na umahiri mdogo au bila umahiri wowote wa kisomo.

Inatupasa

1. Kujua umahiri wa kisomo wa washirika wetu / jamii
2. Tusiwabague wale wasio na kisomo
3. Kutumikia maandishi yaliyo bora kwa 'wasikizaji' wetu
4. Kutumikia mbinu ya 'Kisomo Rafiki' (Tazama hapo chini)
5. Kushirikisha watu katika mazoezi muafaka katika kuendeleza umahiri wa kisomo.

Kwa mfano, mradi wa UKIMWI utakuwa wa kufaa zaidi ikiwa kuna maandishi yaliyochapishwa yaliyo katika lugha rahisi na mradi wa elimu ya wapiga kura unawashirikisha wapiga kura ikiwa wahiriki wa kawaida katika jamii wataweza kusoma fomu za usajili wa wapiga kura.

Mbinu za 'Kisomo Rafiki'

Kwa mbinu zaa 'kisomo rafiki' tunamaanisha kutumia kimaakini vitendo via kusoma na kuandika ili watu watumie umahiri wao wa kisomo na pia kunyosha kidogo. Hii huenda ikajumuisha

- Mwanzoni kuchora ramani za jamii bila maneno, kisha kuongeza maneno machache tu, kama shule, kanisa, kisima ambayo yameandikwa wazi karibu namichoro- vielelezo ili kusaidia walio na umahiri mdogo wa kisomo kushikanisha kwa urahisi maneno na picha.
- Kuuliza kikundi kubainisha maneno muhimu kutoka kwa hadithi ambayo wangeweza kuwa na matatizo ya kuyandika na kuwataka wasaidiane.

Njia nyingine ya kusaidia kisomo wakati wa kusimulia hadithi ni kwa kuuliza watu kusimulia hadithi zao katika vikundi vidogo halafu vikundi hivyo vichague hadithi moja watakayosimulia kikundi kizima kwa kutumia maneno machache, labda vifungu sita pekee.

Baadhi ya hadithi katika kijitabu hiki zilipatikana kwa kutumia mbinu hii rahisi.

Hadithi Katika Vifungu Sita Vya Maneno

Madhumuni

Kuwezesha watu kushiriki matukio muhimu katika maisha yao katika fomu rahisi.

Kitendo

- Katika vikundi vidogo, washiriki wachague hadithi, kwa mfano kutoka kwa mda madhubuti ama kitendo cha mchoro wa ramani
- Pamoja watengeneze vifungu sita vya maneno vinavyo simulia hadithi na kila mmoja aviandike kiviake.
- Kisha kikundi kishirikishe vikundi vingine kwa hadithi yake na kujadili masuala muhimu.

Maelezo kwa Mwezeshaji

Kitendo hiki hufanya kazi vizuri, watu wawe na viwango vya juu au vya chini vya kisomo. Hatua za kukata shauri kuhusu vifungu sita vya maneno hulazimisha kikundi kubainisha maneno muhimu. Matokeo yake ni ya kwamba hadithi mara kwa mara huwa na nguvu mno na hata kuwa chanzo cha majadiliano mengi na vitendo vya kujenga amani.

Ikiwa usimulizi wa hadithi utatumwa katika duru ya kisomo au darasani, hadithi inaweza kutumiwa kama msingi wa vitendo vingi. Kwa darasa wanagenzi, maneno rahisi yanaweza kuchaguliwa na kikundi cha jamaa kijengwe, ikiwezekana, katika lugha asili.

Kwa mfano, neno **bunduki** huenda kikachaguliwa kutoka kwa hadithi, ambalo washiriki watalijenga katika kikundi cha jamii nzima inayomalizikia na **-ki**;

bunduki

mkuki

nyuki

haki

Maneno hayo yanaweza kufanya kuwa vifungu, au kushikamanishwa kuwa hadithi.

Askari alipolenga **bunduki** yake, tulikimbia. Naye hasibu akaturushia **mkuki** aliokuwa nao. Njiani tulipokuwa tukikimbia, tulikumbana na **nyuki** wakali. Kilio chetu ni kupewa **haki** yetu.

Kwa kikundi kipevu cha wanafunzi wa kisomo, washiriki wanaweza kufanya kazi katika vikundi vidogo, mwanzo kwa kuandika moja wa hadithi zao wenye. Halafu waliosalia katika kikundi hicho watajadili watakachokifanya baadaye kitakacho jenga amani katika jamii nahadithiyao fupi kufwata.

Mawazo zaidi kuhusu vitendo wa kisomo na kujenga amani yanaweza kupatikana katika kitabu kii twacho *Integrating Literacy and Peacebuilding: A guide for trainers and Facilitators, 2004* au kwa kusafura [www.balid.org.uk / literacy.htm](http://www.balid.org.uk/literacy.htm)

Hadithi na Mashairi

Hadithi na mashairi yafuatayo yameandikwa na washirika wa Feed the Minds mwakani 2010. Wingi wazo zilisimuliwa wakati wa warsha ya Kotobi, Sudan Kusini, baadhi zao zikasitawishwa ya baadaye.

Baadhi ya hadithi hizi zilisimuliwa awali kwa sauti kubwa katika vikundi vidogo ambayo vilivyokuwa pamoja na wavezeshaji kadhaa wa kisomo. Baadaye kikundi 'kikaweka' hadithi kwa vifungu vifupi vya maneno, pia vichache, vilivyonumiwa katika duru za kisomo.. Katika visa vingi, mihtasari mfupi hii ina uwezo sawia na hadithi ndefu.

Ingawa wingi wa hadithi hizi husimulia shida, maumivu, huzuni na hasara, watunzi wote wameweza kujenga upya maisha yao na ni wanachama watendaji wa mashirika yasiyo ya serikali katika jamii zao, wanachangia vyema katika njia nyingi kama wajenzi wa amani.

Vita ni Vikatili

Hii ni hadithi ya kutekwa nyara na kupoteza ya ndugu zangu
Kijiji chetu kilishambuliwa na waasi
Watu wote 16 wa jamaa yetu walichukuliwa na waasi na kutuhumiwa kuwa
wanashirikiana na serikali
Kati ya watu 16, wanaume 6 waliuawa
Hao 6 walikuwa ndugu zangu wote
Kumbukumbu ya kupoteza bado ni chungu kwetu

Yotoma James, Kotobi, Sudan Kusini, Mei 2010



Maswali ya kujadiliwa na vikundi:

1. Ni madhara gani matukio haya unafikiri jamaa wa Yotoma walipata?
2. Unadhani Yotoma anahisi nini kuhusu kunusurika?
3. Jamaa itawakumba vipi watu wao waliopotea?

Maneno Muhimu: migogoro, kupoteza, huzuni, uponyaji, upatanisho

Kupambana na Unyanyapaji

Mimi ni yatima, nilipoteza wazazi wangu na UKIMWI
Baba yangu alikuwa dereva, alindesha lori kutoka Kampala kwenda Arua
Alikuwa na mwanamke kijana sana ambaye alimuambukiza ugonjwa
Alikataa kwenda kupimwa
Na akafa mwakani 1996 katika njia isioelewaka
Mwishoe tumeteseka sana
Baadhi yetu tukikosa kuelemishwa

Dada yangu anaishi na mimi na hunisaidia kumtunza binti yangu
Ninamfundisha kusoma na kuandika.

Gasi Stella, Kotobi, Sudan Kusini, Mei 2010
Kutokana na Matukio Kaskazini mwa Uganda

Maswali ya Kujadiliwa na Vikundi:

1. Stella na jamaa yake waliteseka vipi kutokana na UKIMWI?
2. Unadhani Stella anahisi nini kumhusu baba yake?
3. Je, unamjua mtu yeyote anayeishi na UKIMWI? Unajiweka vipi unapokuwa nao? Ni nani mwagine anayebaguliwa katika jamii yako?
4. Je, unajua jinsi ya kujua hali yako ya UKIMWI?

Maneno Muhimu: ubaguzi, msamaha, usawa wa kijinsia/wanawake, huzuni, uponyaji, hasara, unyanyapaji

Anyimwa Elimu kwa Ajili ya Ndevu Zake

Baba alipokuwa shuleni, vita vilikazuka

Vita vikakoma

Baba kurudi shuleni

Mwalimu alikataa kumruhusu kukaa

Alikuwa amemea ndevu

Akatumwa kurudi akaoe

Christopher Malone, Kotobi, Sudan Kusini, Mei 2010

Kutokana na Matukio ya Vita vya Sudan

Maswali ya Kujadiliwa na Vikundi:

1. Unamjua nani aliyekosa elimu kutokana na migogoro?
2. Kuna ubaguzi gani katika hadithi hii?
3. Ikiwa mtoto wako angekatazwa shule ungeweza kwenda kwa ushauri?

Maneno Muhimu: elimu ya uraia, vita, ubaguzi

Je, Nilichagua Vyema?

Hapakuwa na daktari wengi wala dawa katika vita
Nilipoteza baba yangu kwa sababu hii
Kisha mme wangu alikuwa mgonjwa na nikaambiwa ni lazima kuwa na dawa kutoka mbali
Nitakaa naye ama nitakwenda kuafuta dawa ili kuokoa maisha yake?
Nilikwenda kutafuta dawa
Lakini akafariki hali niko mbali bila mimi karibu naye
ilinivunja moyo kwa kutokuwa huko.

Gertarude Filipo, Kotobi, Sudan Kusini, Mei 2010
Kutokana na Matukio ya Vita vya Sudan



Maswali ya Kujadiliwa na Vikudi:

1. Ni sehemu gani mgogoro ulitekeleza katika kila moja ya vifo ya baba na mume wake?
2. Nini huduma gani za afya zilizoko sasa katika jamii yako?
3. Ufikiri Gertarude atajenga upya maisha yake vipi ?

Maneno Muhimu: migogoro, hasara, huzuni

Teksi, Tafadhal!

Bw. Fred Mugerwa ni mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Makerere. Ana ulemavu wa mwwili.

Siku moja Fred alikuwa njiani kwenda kwake nyumbani mjini Kampala alipokatazwa teksi. Dereva teksi alimfokea, ‘Sina muda na watu wasio na maumbile mema.’ Watu wengine waliruhusiwa kuingia katika teksi na hakuna mtu aliyemsaidia Fred aliposukumwa nje ya teksi.

Fred ni mwanachama wa shirika lisilo la serikali liitwalo *Youth with Physical Disabilities Development Forum (YPDDF)*. Alijua kwamba kuna sheria nchini Uganda na kimataifa zinazolinda haki za watu walio na ulemavu na akaamua kutafuta haki. Kwa ushauri YPDDF, Fred akaenda Polisi wa Uganda na Tume ya Haki za Binadamu na akaweka malalamishi yake dhidi ya kampuni teksi ya Uganda.

Kampuni ya teksi ikampatia Fred mlungula wa fedha ili kutatua kisa hicho. Fred akakataa kupokea malipo kwa sababu alitaka kampuni ya teksi ipatikane na hatia mahakamani ili kisa hicho kiwe funzo kwawengine.

Henry Nyombi, Youth with Physical Disability Development Forum
Kutokana na Matukio Uganda

Maswali ya Kujadiliwa na Vikundi:

1. Ni aina gani ya ubaguzi umefanyika? Unadhani Bw. Mugerwa alihisi nini alipokatazwa kuingia katika teksi?
2. Je, umeshawahi kubaguliwa? Ungelienda kupata usaidizi?
3. Je, ungepokea pesa za mlungula alizopewa Fred na kampuni ya teksi, au ungepeleka kisa hicho mahakamani?

Maneno Muhimu: elimu ya uraia, ubaguzi, unyanyapaji

Nalia Kinyamavu

Nyayo nzito zangia kwa nyumba
Moyo wangu wapiga kasi
Mama yangu apiga mayomwe dakika chache baadaye
Mara nyayo hizo zaondoka baadaye!

Nalia kinyamavu na kujaribu kulala
Ni lazima niende shulenii kesho
Ninashangaa kwani baba humpiga mama yangu.

Judy Amunga, Tatua Communications, Agosti 2010
Kutokana na Matukio Kenya



Maswali ya Kujadiliwa na Vikundi:

1. Unafikiri ni kwa nini mtu humpiga mwanamke katika hadithi hii?
2. Je, unafikiri watoto watahisi nini?
3. Ni nani katika jamii yako anaweza kusaidia jamaa hii?

Maneno Muhimu: kutokuwa sawa kwa kijinsia/wanawake, huzuni, hasara, mgogoro

Majirani katika Amani

Mimi ni mtu anayeweza kufanya amani
Nampenda nchi yangu sana,
Nawezaje kumuua ya jirani yangu,
Wakati ye ye ni binadamu kama mimi?

Kwa nini ni jirani yangu anakufa na njaa,
Njaa,
Nami nina chakula?

Nasimama chini ya juu,
Lililozungukwa na nyota,
Kuapa kwamba kamwe sitakuacha na njaa, jirani yangu!

Boniface Ambani, Kibera, Kenya, Agosti 2010
Kutoka kwa kumbukumbu yake akiwa na umri wa miaka 13

Maswali ya kujadiliwa na Vikundi:

1. Majirani katika jamii yako huchukuliana vipi?
2. Unawezaje kumsaidia jirani yako?
3. Jirani yako atakusaidia wewe na jamaa yako?

Maneno Muhimu: migogoro, maridhiano, amani, uponyaji

Elimu ni Ufunguo wa Amani

Maria aliishi katika kijiji cha mbali ambako kuelimisha watoto wa kike haikuwa muhimu. Watu walipenda Maria kwa moyo wake mpole na kazi alioifanya kanisani, lakini alikuwa hajawahi kwenda shulen. Rafiki yake Gloria alikuwa ana elimu kwa sababu baba yake alikuwa mwalimu wa shule.

Mwalimu, kwa jina Petro, akampenda Maria akitaka amuo. Wazazi wao walikubaliana kuhusu mahari. Baada ya kuchumbiana, Petro ilipata fursa ya kwenda Ufaransa kwa masomo zaidi. Kabla ya kwenda, walikubaliana kuwasiliana kuhusu maandalizi ya harusi. Kidogo, Petro kujua kwamba Maria hakujuwa kuandika au kusoma vizuri.

Petro alimuandikia Maria kutoka Ufaransa kumweleza jinsi nchi hiyo ilivyokuwa nzuri na jinsi alivyomkosa. Maria alimkimbilia Gloria akasomewe barua zake. Ingawa Maria alimuamini Gloria, Gloria alimwonea wivu Maria ambaye alikuwa aolewe na mtu aliye elimika na kufikiria angelikuwa ni yeye.

Gloria akabuni maneno mabaya ya kuumiza Maria na kumhasimisha dhidi ya Petro. Maria akawa na kiwewe, akidhani Petro hakumpenda tena. Akakimbilia mama yake kumwambia aliyosema Gloria kuwa yalikuwa katika barua kutoka kwa Petro. Mama yake alijua Gloria alikuwa ndiye msichana wa pekee aliyeelimika katika eneo hilo ambaye alitaraji Petro awe mume wake. Akashuku huenda ikawa Gloria alikuwa anamdanganya Maria.

Yeye akamliwaza bintie na kuntia moyo ajiunge na darasa la kisomo cha watu wazima ambalo lilikuwa mbali kidogo kutoka nyumbani kwao. Maria akajihatarisha na kujiunga na darasa la kisomo. Taratibu, alijifunza kusoma na kuandika. Alipozisoma barua kutoka kwa Petro, aligundua kuwa aliya ambiwa na Gloria haikuwa kweli.

Akaamua kumuandika Petro yeye mwenyewe, kumueleza kilichotokea. Aligundua polepole kuwa angeweza kusoma barua za Petro na kuandika baadhi wazo mwenyewe. Wakaweza kupatanishana na kupanga harusi yao.


Felicien Nemeyimana, Kotobi, Sudan Kusini, Mei 2010
Kutokana na Matukio Rwanda

Maswali ya kujadili wa na

Vikundi:

1. Tunaweza kuelezea uhusiano kati ya Maria na Gloria ulikuwaje?
2. Mama yake Maria alichangia nini katika uhusiano huo?
3. Utawashauri nini wazazi wanaowanyima watoto wao elimu?
4. Jinsi gani kisomo kinaweza kuwa chombo cha maridhiano na uponyaji?

Maneno Muhimu: usawa wa kijinsia /wanawake, upatanisho, amani



Wanawake Wamesimama Pamoja

Kulikuwa na mwanamke aitwaye Gladys aliyeishi katika kijiji kidogo. Angeweza kusoma na kuandika kidogo tu, lakini alikuwa mtaratibu na mpole. Ulipowadia wakati wa kulima, alilima shamba lake mwenyewe, kisha angepanga wanawake wachanga walime mashamba ya wanawake ambao hakuweza kufanya hivyo wenyewe. Wanawake waliokuwa na ulemavu au wale vikongwe walitunza watoto pindi mashamba yao yalipokuwa yakilimwa.

Wakati ulifika wa kuchagua kamati ya elimu na wanawake wakamwambia Gladys, "Ni lazima tuwe na mwanamke katika kamati. Utatusimamia?" Gladys akubali na jina lake mbele.

Kukawa na mkutano na mwanamme mmoja akasema, "Gladys, wewe ni mpole na unaweza kupika vyema. Lakini hauwezi kusoma na kuandika vizuri. Hivyo basi, hauwezi kuwa katika kamati ya elimu." Wanaume wengine walikubalina naye. Kura zilipopigwa, zilifanyika kwa kunyoosha mikono juu. Wanawake wakahofia sana kumpigia kura Gladys kwa sababu ya yaliyosemwa kumhusu na wale wanaume. Kwa hivyo Gladys hakuchaguliwa.

Gladys aliuliza rafiki zake, "Kwa nini hamukunipigia kura?" Wakasema, "Je, haukuona jinsi Mkuu wa Lokesheni alinitazama kwa jicho lake?" Gladys rafiki zake wakahuzuni. Kamati ya elimu ikawa nawanaume peke yake.

Mwaka ulifwata jamii hiyo ilipokea mafunzo ya elimuya uraia, uchaguzi wa viongozi na umuhimu wa maoni ya wanawake na watu walio na ulemavu kusikika. Kura zilipigwa kwa siri. Kila mmoja wa wagombea viti iliwalishwa na harage au mbegu. Kila mtu ilichukua harage au mbegu moja na kuiweka katika mtungi wa kura.

Mara hii wanawake hawakuogopa na Gladys akachaguliwa. Sasa kazi ingeanza ili kufanya masuala ya wanawake na kujadiliwa.

Katy Newell-Jones, Kotobi, Sudan Kusini, Mei 2010
Kutokana na Matukio Cameroon

Maswali ya Kujadiliwa na Vikundi:

1. Je, chaguzi hizo zilikuwa za kidemokrasia na adilifu?
2. Ni ubaguzi gani ulikuwepo katika hadithi hii?
3. Mnachagua namna gani viongozi katika jamii yako?

Maneno Muhimu: elimu ya uraia, ubaguzi, usawa wa kijinsia

Uponyaji Kupitia kwa Msamaha

Baba yangu alikuwa na wake kadhaa.jamii yote nzima ilisimamiwa na mke wa kwanza aliye kuwa ndiye wa halali, hivyo basi, watoto na wajukuu wake walinufaika. Walifaidika na chakula, elimu, mavazi na mahitaji mengine ya kimsingi. Palikuwa na migogoro minge katika jamii.

Hapa nikinyimwa elimu, masomo ya kaka yangu yalifadhiliwa na baba yetu. Lakini kwa azma ya mama yangu, na kwa usaidizi wa mmisionari na dada yangu mmja, nilipata elimu yangu. Hapakuwa na dada yangu aliye enda shulen i kirefu.

Wakati wa vita va ukomboziwa DRC ulizuka, kaka aliahidi kupatia jamii yangu yote usafiri, lakini akachukuwa jamaa yake pekee. Dada zangu na mimi tukaachwa ukiwa, twasononeka na wakudhuriwa.

Vikosi vilipokuja kijijini kwetu, walitupata nyumbani na wakawachukuwa dada zangu. Dakika chache baadaye, walirudi nakunichukuwa na wakanilazimisha kuwa angalia dada zandu wakibakwa kikatili.

Mwanajeshi mmoja mwanamme alikuja akatuokoa na akayupeleka kwenye makazi ya majeshi. Lakini dada yangu mmoja alikataa kwenda pamoja nasi. Baadaye nilirudi kumtazama lakini nikapata kuwa alijinyonga.

Tulikaa kwa mda wa miaka miwili katika kambi ya wakimbizi. Nikaregeshwa nyumbani ambako nilimpata kaka yangu na sasa maridhiano yanafanyika pole pole. Hata hivyo, majeraha makubwa yalioachwa yatachukuwa miaka minge kupona.

Ekombe Adhumani, kotobi, Sudan Kusini, Mei 2010
Kutoka kwa Matukio katika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

Maswali ya Kujadiliwa na Vikundi

1. Ni kwa jinsi gani haki za wanawake zilitukanwa?
2. Ni kwa jinsi gani Adhumani alijenga upya jamaa yake?
3. Ungelihisi nini ungelikuwa Adhumani?
4. Chanzo cha migogoro katika jamii kilikuwa nini?

Maneno Muhimu: Migogoro, ubaguzi, Kufurushwa, msamaha, kutokuwa na usawa wa kijinsia, hasara, amani, maridhiano

Mpango wa Hatua Tano

Feed the Minds imetengeneza mpango wa kutumia kisomo kwa kuimarisha miradi yote.

1. Kiwango cha kisomo	<p>Watu wa mtaa wana kiwango gani cha kisomo?</p> <p>Wanawake hutumia vipi kisomo na herufi?</p>
2. Epusha kusononeka na ubaguzi	<p>Je, tunawazuia watu wasiojua kusoma na kuandika wasiwe katika warsha, mafunzo au nafasi za uabikaji? Yunafanya nini ili kuhakikisha kuwa watu wasiojua kusoma na kuandika wanhusishwa katika vitendo vyatmiradi?</p> <p>Je, vitu vyetu vyatmiradi vimekuwa kizuizi cha watu walio na kiwango duni cha kisomo?</p>
3. Kagua na utumikie vitu vilivyoandikwa	<p>Je, tunatumia maneno na vifungu vyatmiradi vimekuwa kizuizi cha watu walio na kiwango duni cha kisomo?</p> <p>Je, tunaweza kutumia picha na mjchoro kueleza hayo? Ni lugha gani itaeleweka na watu wengi?</p>
4. Kunakowekana endeleva umahiri wa kisomo	Sio lazima tuwe wavezeshaji wa kisomo ili tuwasaidie washiriki kuendeleza umahiri wao wa kisomo.
	<ul style="list-style-type: none"> • Tambua maneno muhimu watakayojifunza washiriki • Soma kwa sauti ya juu maandishi yalioandikwa kwa ubao • Gawa maneno magumu • Sisitiza sauti ya herufi ya kwanza • Tumia mchanganyiko wa herufi wala usitumie herufi kubwa pekee
5. Shirikisha mawazo yako katika kuimarisha kisomo	<p>Je, waalimuna, wavezeshaji na mashirika wamewashirikisha watu wengine wa shirika letu katika umahiri na matukio yao?</p> <p>Je, shirika letu limeshirikisha vitendo na mawazo mema kwa ajili ya kuimarisha kisomo na mashirika yasio ya serikali?</p>

Tajo

Hapa chini pana baadhi ya tajo za manufaa katika kutumia kisomo na usimulizi wa hadithi kwa ajili ya kujenga amani, kuponya sononeko, na elimu ya uraia. Tajo hizi zote zaweza kupatikana kwa kusafura tuvuti bila malipo.

- Integrating Literacy and Peacebuilding: A guide for trainers and facilitators. Sam doe, Juliet McCaffery & Katy Newell-Jones. Education for Development, 2004.
Tuvuti: www.balid.org.org.uk/literacy.htm
- Her Stories: A collection of women's stories from Africa. Action Aid, 2010.
Tuvuti: www.acctionaid.org/main.aspx?PageID=1424
- Education for all – Global Monitoring Report 2010: Reaching the Marginalized. UNESCO.
Tuvuti: <http://www.unesdoc.unesco.org/images/0018/001866/186606e.pdf>

PERSONAL NOTES

